# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA

## MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKONO KWA KIDATO CHA KWANZA 2021

**JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………………………………………..**

**JINSI…………….............................................**

1. **Ninayo furaha kubwa na kukupongeza kwa ufaulu wako na kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mkono mwaka 2021. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 na unatakiwa kufika shuleni siku hiyo kwani masomo yanaanza tarehe hiyo kwa <u>ENGLISH ORIENTATION COURSE</u> na baada ya kozi hii kutakuwa na mitihani ya upimaji.**
2. **MAHITAJI YA SHULE**
    - **ADA NA MICHANGO; Hakutakuwa na ada wala michango ya aina yoyote utakayotakiwa kuchangia shuleni.**
    - **SARE YA SHULE;**
        - I. **Suruali mbili moja ya DAMU YA MZEE na nyingine NYEUSI kwa wavulana. Suruali hizi zishonwe kwa unadhifu na ziwe na marinda mawili na mifuko mshazari miwili mbele na mmoja nyuma. Suruali za kubana(modo) ni marufuku na atakayekuja na suruali ya aina hii atanyang'anywa na suruali hiyo itachomwa moto.**
        - II. **Sketi mbili kwa wasichana moja DAMU YA MZEE na nyingine NYEUSI. Sketi hizi ziwe za kitambaa kizito na zishonwe zikiwa na marinda sita na zenye upana wa kutosha. Pia ziwe ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu.**
        - III. **Shati mbili nyeupe mikono mifupi zisizo za kubana kwa wavula na wasichana. Mashati haya yapigwe nembo ya shule ya sekondari Mkono kwa utambulisho.**
        - IV. **Soksi jozi mbili nyeupe kwa wavulana na wasichana. Soksi zote zinatakiwa ziwe ndefu kwa wavulana na wasichana.**
        - V. **Sweta mbili ya Moja Damu ya Mzee na nyingine blue yenye mikono mirefu na shingo ya V kwa wavulana na wasichana.**
        - VI. **T- shirt ya Rangi ya Njano yenye nembo ya shule ya sekondari Mkono. T-shirt hii itavaliwa siku ya michezo tu na si vinginevyo.**
        - VII. **Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu na vyenye kamba.**
3. **MAHITAJI YA DARASANI.**
    - I. **Madaftari makubwa aina ya conter books kuanzia quire two yasiyopungua kumi.**
    - II. **Mathematical set, kalamu nyeusi au blue za kutosha, penseli na ufuto na rula**
    - III. **Ream. DOUBLE A ( mwanafunzi awe nayo nyumbani ataileta shuleni pindi ukihitajika)**
    - IV. **DICTIONARY(Pia mzazi au mlezi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vya masomo mbalimbali kwa ajili ya rejea binafsi)**
    - V. **FOLDER FILE(kwa ajili ya kumbukumbu binafsi za mwanafunzi)**
4. **MATIBABU;**

    **Shule haitatoa matibabu kwa mwanafunzi pindi anapougua. Jukumu la matibabu ni la mzazi/ mlezi. Hata hivyo shule inaweza kutoa huduma ya kwanza pale mwanafunzi awapo shuleni kabla ya kuchukuliwa na mzazi/mlezi kwenda kwenye tiba.Uongozi wa shule unashauri mzazi kulipia sh 5000 ili tuwatengenezee bima ya afya ya kaya.**
5. **SHERIA ZA SHULE**

    **Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha Shule inazingatia miongozo mbali mbali inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknologia na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo unatakiwa kuzingatia yafuatayo.**
    - **Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.**
    - **Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na N je ya shule ni muhimu.**
    - **Kuwahi shuleni SAA 12:45 asubuhi na kuhesabu namba.**
    - **Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani n nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako.**
    - **Kuzingatia usafi wa mwili na mazingira ya shule**
    - **Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa ndani ya shule na unapokuwa nje ya shule kwa ruhusa.**

- **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**

**6. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANANZI KUFUKUZWA SHULE.**

- **Wizi**
- **Uasherati, ushoga na ubakaji**
- **Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya**
- **Kupigana au kupiga**
- **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma**
- **Kudharau bendera ya Taifa**
- **Kuoa au Kuolewa**
- **Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba nje na ndani ya shule**
- **Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu**
- **Kukataa adhabu kwa makusudi.**
- **Mwanafunzi kumiliki au kuwa na simu ya mkononi ndani na n je ya shule**

**KARIBU SANA MKONO SEKONDARI**

**SAMSON ORINGA**
**MKUU WA SHULE YA MKONO SEKONDARI**
**0755419792/0674216198**

**FOMU HII IRUDISHWE SHULENI KWA MKUU WA SHULE WAKATI WA USAJILI**

**FOMU YA MAELEZO JUU YA MWANAFUNZI**

Jina la Mwanafunzi …………………………………………..liwe jina ulilolitumia katika shule uliyotoka na utalitumia kwa miaka yote utakayokuwa hapa shuleni na huruhusiwi kulibadili.
Dini…………………………………………. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………….
Nambari ya kuingizwa shuleni……………… Shule aliyotoka ……………………………………………
Tarehe…………………………. Michezo uipendayo au shughuli uzipendazo (hobbies) ……………………………………………………………..
Kipimo au historia ya ugonjwa …………………………………………………
Unaishi na nani/uhusiano …………………………………………………………
Jina na anwani ya kudumu ya mzazi/mlezi atakayetumiwa ripoti ya maendeleo yako ya kitaaluma na tabia………………………………………………………………………………………
Kazi ya mzazi/mlezi………………………………………………………..
Mahali ……………………Wilaya …………………………Mkoa ……………………………
Habari nyinginezo ………………………………………………………………………..
Mzazi /mlezi aliye hai ……………………………………………………………….

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi mwenyewe.
Mawasiliano ya Mzazi/mlezi na ndugu wa karibu

| S/NO | JINA | UHUSIANO | NO.SIMU | ANAKOTOKA | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |
| 4 | | | | | |

Sahihi ya mzazi /mlezi ………………………tarehe……………………….. simu…………………………
Mimi (jina la mwanafunzi) ……………………………….. ninaahidi kuzingatia utaratibu, Kanuni na sheria za shule bila kukiuka. Kinyume na hayo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu. Nitasoma kwa bidii na kufanya kazi ninazotakiwa ili kufikia lengo linalotakiwa.
Sahihi ya mwanafunzi………………………….. tarehe…………………………………..

**FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAE KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MKONO**

1. Mimi ……………………........ Baba/Mama/Mlezi wa …………………………..
Ninayeishi Wilaya …………………… Mkoa………………………… nakubali mwanangu ……………………… ajiunge na shule ya sekondari ya Sekondari MKONO.

2. Mimi mzazi/Mlezi wa kijana huyu naahidi kushirikiana na walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule. Kwamba ni wajibu wangu kama mzazi/mlezi kumuhimiza mwanangu asome kwa bidii na afuate sheria na taratibu zote za shule.

3. Nitamhimiza mwanangu kuhudhuria masomo kila siku za masomo na endapo atashindwa kufika shuleni bila taarifa nitalipa faini ya utoro sh. 5000 kwa kila siku atakayokosa masomo. Na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia.

.

Jina la mzazi/mlezi………………………………………….
Sahihi ………………………………….. Tarehe……………………………………..

**MKONO SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 475, MUSOMA - MARA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR THE STUDENT**
**(To be filled in the Government hospitals only)**

1. Student's name……………………………………………….. Age………………………
2. Please examine the above mentioned student to her fitness for joining advanced level studies in the following test:-

i. Blood examination Haemoglobin ………………………………………………….
ii. Stool examination………………………………………………….
iii. Bilharziasis……………………………………………
iv. Urinalyisis………………………………………………
v. Tuberculosis Test (TB)…………………………………………..
vi. Eye……………………………………………………
vii. Abdomen ……………………………………………………………..
viii. Athma …………………………………………………….
ix. Headache…………………………………………………
x. Inability to eat certain type of food ………………………………………………………
xi. Skin disease …………………………………………………,
xii. Pregnancy ……………………………………………………
xiii. Any abnormalities noted………………………………………………..
xiv. Any chronic complains noted above ………………………………………………….
xv. Anything else that the school health staff should know about
……………………………………..
xvi Any treatment given or
recommended……………………………………………………
xvi. Any STD detected ………………………………………………………………….

Note: In case of unhealthy detected, it is recommended that a student should get treatment before coming to school.

I have examined the above student and consider that she is physically fit for joining advanced/ordinary level studies.

Signature of the Examiner ……………………………………………………
Designation ……………………………………………………
Station …………………………………………...
Date ……………………………………………………..